24.2 KISWAHILI (102)

24.2.1 Kiswahili Paper 1 (102/1)

MANYAM FRANCHISE
Discover!Learn!Apply

Swali la Kwanza

Muundo

1. Kichwa
   - Kiteuliwe kulingana na mada husika.
   - Kitaje mada na tarehe.(muda ambao kamati ilifanya kazi).
   - Kiandikwe kwa herufi kubwa na kipigiwe mstari.(Udhaifu ushughulikiwa ki-mtindo).
2. Utangulizi
   - Mwandishi atoe usuli mfupi au maelezo ya jumla kuhusu mada ya ripoti au historia fupi ya shughuli husika.
3. Mwili
   - Uelezee maudhui, ripoti itumie nafsi ya tatu, kauli ya kutendewa na wakati uliopita.
   - Inaweza kuwa na visehemu vyenye vichwa vidogo vidogo.
4. Hitimisho
   - Alipotumia wakati au nafsi aondolewe zw(wakati) hapo mwisho baada ya kutuza.
   - Aeleze japo kwa ufupi mambo muhimu katika ripoti. Aweza kutoa ushauri au mapendekezo kuhusu mada iliyoshughulikiwa kwa kuagiza mambo ya kufanywa au kukataza yasiyofaa kufanywa.
5. Jina la mtayarishi, sahihi na tarehe.(siku ya kuandika ripoti)

Kwa mfano:

Muundo wa ripoti uzingatie

a) Utangulizi: kichwa: kupambana na dawa za kulevya.

b) Dawa za kulevya
   - Dawa ambazo zina athari mbaya kwa afya.
   - Dawa zinazotumiwa vibaya.
   - Dawa zenye athari ya uraibu: mairungi, mihadarati, bangi, sigara, pombe.

c) Athari zake:
   - Huathiri afya ya mtumiaji.
   - Hujenga uraibu mbaya.
   - Huathiri utenda kazi wa mtumiaji.
   - Huwa chanzo cha mabadiliko ya kitabia.
   - Huuharibu ubongo wa mtumiaji.
   - Humzuga/humtawala mtumiaji kiasi cha kutoweza kufanya lolote bila kuzitumia.
   - Huwa na athari kwenye jamaa na jamii.
   - Huwa chanzo cha maovu mengi ya kijamii.

Powered By: www.manyamfranchise.com

Mapendekezo:

- Uelimishaji wa jamii kuhusu madhara yake.
- Kutumia vyombo vya habari kama redio na runinga.
- Matumizi ya mabango katika maeneo mbalimbali.
- Kuhusishwa kwa elimu inayolenga madhara yake katika mtaala.
- Kuandaliwa kwa semina za kuhamasisha umma.
- Kusambazwa kwa maandisi ambayo yanalenga kuwaelimisha wanajamii.
- Kutumiwa kwa vyombo vya sheria.
- Kupambana na watumiaji.
- Kuwepo kwa vituo vya kuwasaidia walioathirika na dawa za kulevya.
- Kuwahusisha wananchi wote kwenye harakati za kupambana.
- Kuhusishwa kwa asasi kama dini (makanisa, misikiti nk) kueneza habari hizi muhimu.
- Kuwepo na nyenzo za kuchunguza na kupambana na dawa za kulevya.

d)Hitimisho: Makubaliano ya kikao

e)Kitambulisho sahihi, hina na terehe.

Swali la Pili

Insha iakisi maana ya ndani ya methali kuwa cheo au mamlaka huwa ni kama mahali pa kutupa takataka. Maana ya ndani: mwenye cheo hulaumiwa au kushutumiwa mambo yanapoenda kombo. Wenye vyeo wasishangae wanapokumbwa na lawama kutokana na hali au matendo fulani. Mtahiniwa aandike kisa au visa kuthubitisha ukweli wa methali. Atakayeegemea upande mmoja atakuwa amepunguki – maudhui. Maelezo, ukubwa, cheo, mamlaka, umri, wadhifa, usimamizi, majukumu. JAA – kulaumiwa, kusingiziwa, kutumiwa, kutusiwa, kushutumiwa, kupigwa, kupigwa vita.

Swali la Tatu

Insha ya kiubunifu ambayo inapima uwezo wa mwanafunzi wa kubuni na kutunga kisa ambacho kinaingiliana na vidokezo vilivyotolewa.

Sifa za Kuchunguza:

Insha iakisi sifa zifuatazo: majuto, maonyo. Yalihusu nini, aliasi namna gani, kwa nini akapuuza maonyo. Matokeo ya haya mapuuza. Athari za haya mapuuza.

i) Asiyemaliza kwa maneno aliyopwea amejitungia swali na kulijibu

ii) Anayeongewa zk(kimalizio) baada ya kutuzwa.

iii) Anayeanza kunakili kimalizio na asilamili aondelewe zk (kimalizo) baada ya kuuzu.

Swali la Nne

Insha ya mjadala.

Utangulizi: Utandawazi au utandaridhi:

Mahusiano ya kijamii, kisiasa na kiuchumi kwa teknolojia yanayokiuka mipaka ya kitaifa na kuufanya ulimwengu kuwa kama kitu kimoja/kijiji kitandaridhi/kitandawazi.

Powered By: www.manyamfranchise.com

Faida za utandawazi

- Kuhimiza maingiliano ya jamii mbalimbali ulimwenguni.
- Kusambaza maarifa kutoka sehemu moja hadi nyingine.
- Kuwa msingi wa elimu na uenezaji wa maarifa muhimu.
- Kuchangia katika kusambaza haki au maarifa ambayo hayapatikani kwingineko.
- Kuharakisha maendeleo katika sehemu mbalimbali za ulimwengu.
- Kuwawezesha watu ulimwenguni kufaidika kutokana na teknolojia bora.
- Kuchangia katika maendeleo ya kiuchumi ya maeneo mbalimbali kutokana na biashara kama utalii.

Powered By: www.manyamfranchise.com

24.2.2 Kiswahili Paper 2 (102/2)

(a) Ufisadi, uongozi mbaya, turathi za kikoloni, uchumi kutegemea kilimo chenye mvua isiyotabirika, idadi kubwa ya watu, nafasi adimu za kazi, madeni.
(alama 4)

(b) Asilimia kubwa ya pato la mataifa yanayoendelea huishia kulipa madeni haya. Hivyo inakuwa vigumu kwa mataifa hayo kujikwamua kutokana na umaskini.
(alama 2)

(c) Kuibuka na mikakati bora ya kupambana na umaskini
Sera zinazotambua kuwa raia wake wengi ni maskini
Kuzalisha nafasi za ajira
Kuimarisha miundo msingi
Kuhakikisha kuwa mfumo wa soko huria hauishii kusababisha kufungwa kwa viwanda.
(alama 4)

(d) Unaweza kuwa chanzo cha kufa kwa viwanda asilia na kuendeleza umaskini zaidi. ***(alama 2)***

(e) (i) Kulitatua
(ii) kuzalisha/kuwa chanzo
(iii) Kuyasamehe madeni ***(alama 3)***

2. (a) Ajira ya watoto ni tatizo
Sababu zake ufukara, gharama za maisha
Ukosefu wa lishe huwafanya watoto kutoroka
Kuna maonevu kwa watoto: aina za maonevu
Janga la ukimwi. ***(alama 7)***

(b) Wanayoyapata huko nje – mateso
Malipo duni
Kujiingiza katika uhalifu – jinai, kupora, biashara haramu
Umoja wa Afrika na unayoshughulikia
Matatizo ya Africa
Haki za watoto
Watoto kama asilimali. ***(alama 8)***

3. (a) Chumvi imemwagika mezani pake
Chumvi imemwagika mezani pao ***(alama 1)***

(b)



(alama 4)

(c) a-li-m-chez-e-a
a-nafsi, umoja, kipatanishi
li-wakati uliopita
m-kiwakilishi cha yambwa
e-mnyamjuliko – fanyia

Powered By: www.manyamfranchise.com

a-mwisho wa kitenzi(hali yakinishi) *(alama 3)*

(d) m,p,b *(alama2)*

(e) Nisingalikuwa na pesa nisingalinunua nyumba *(alama 2)*

(f) Kutendata *(alama 1)*

(g) (i) Maria alicheza ngoma Mombasa *(alama 1)*
(ii) Mkulima alifika nyumbani asubuhi *(alama 1)*

(h) (i) Tuzo ilishindwa na mhunzi mrefu *(alama 1)*
(ii) Yuyu huyu mwanafunzi anasoma kifaransa *(alama 1)*

(i) (i) Sahili *(alama 1)*
(ii) Ambatano *(alama 1)*

(j) Peter alishindwa katika riadha seuze wewe? *(alama 1)*

(k) Jirani mwema – kirai nomino
Alinipa chakula – kirai tenzi *(alama 2)*

(l) Kuchelewa/uchelewaji *(alama 1)*
Kuandika/mwandiko/uandikaji *(alama 1)*

(m) (i) Uwezekano *(alama 1)*
(ii) Mazoea *(alama 1)*

(n) Japo Selina alijitahidi sana hakushinda mbio hizo *(alama 1)*

(o) Mwise alikunjua nguo alizokuwa ameanua *(alama 2)*

(p) Mtoto niliyemsomesha ameasi jamii
Mtoto ambaye nilimsomesha ameasi jamii *(alama 1)*

(q) Mkolwe alisema kuwa hangethubutu kumpa pesa zake *(alama 2)*

(r) Msusi anasuka nywele vizuri
Jambo jipya limezuka nchini mwetu *(alama 2)*

(s) Hutumiwa mahali ambapo sauti imedondoshwa *(alama 2)*

(t) Kijikiti
Jikiti *(alama 2)*

(u) Kiunganishi
Kihusishi *(alama 2)*

4. (a) (i) Muktfadha wa mahakamani. Hii ni lugha ya kisheria. *(alama 1)*

(b) Matumizi ya msamiati unaorejelea sheria kama vile: sheria, kifungsu nambari 3 sehemu ya A.....nk, sheria za nchi, umepatikana na hatia. Sentensi aghalabu katika lugha ya kisheria huwa ndefu. Kifungu hiki kina sentensi ndefu sana. mf sentensi ya kwanza na ya tatu.

Vifungu vya sheria vimewekewa nambari mf. Sheria kifungu nambari 3 sehemu ya 4, hili husaidia kurejelea kifungu kinachotajwa ili kuweza kutetea uamuzi au kauli fulani. *(alama 3)*

(c) Lugha yenye kaida zake

Lugha yenye unyenyekevu na heshima. Aghalabu hakimu au jaji lazima atambulishwe kwa "mheshimiwa hakimu au mheshimiwa jaji" mtuhumiwa husikika akisema " Naomba mahakama inihurumie au inifanyie hiki na kile".

Powered By: www.manyamfranchise.com

Lugha ya mzaha au inayoleta vichekesho haihitajiki na huenda ikamkera hakimu.

Sarufi huchujwa kirasmi. Katika sheria kila neno au muundo wa sentensi lina umuhimu wake. Neno linalotumika hutumika kwa makini ili maana yake iwe wazi kwa wote.

Lugha hii haitakiwi kuwa na utata wa aina yoyote.

Lugha hii zaidi hulenga wataalamu walioelimika kisheria. Mara nyingi mtu wa kawaida huhitaji mtaalamu kumrahisishia yale yanayoendelea. ***(alama 6)***

Powered By: www.manyamfranchise.com

24.2.3 Kiswahili Paper 3 (102/3)

1. (a) Fasihi simulizi ni sanaa ya lugha inayohusu masimulizi au utendaji kwa njia ya mdomo. Fasihi hii imekuwa na binadamu tangu alipoanza kuishi. Imekuwa ikirithishwa kizazi kimoja hadi kingine. *(alama2)*

(b) Tofauti baina Fasihi simulizi na Fasihi andishi

	Fasihi simulizi		**Fasihi andishi**
(i)	Huwasilishwa kwa njia ya mdomo na vitendo	(i)	Nyenzo za uwasilishaji ni maandishi
(ii)	Yaweza kutungwa na kutenda papo kwa papo.	(ii)	Hutungwa kwa kipindi kirefu cha wakati
(iii)	Huwa ni mali ya jamii na haina mmiliki mmoja	(iii)	Huwa ni milki ya mtu mmoja ama walioandika
(iv)	Hadhi yake ni hai na huweza kushirikishwa kikamilifu katika utendaji	(iv)	Hadhira yake ni tuli kwani ni wenye uwezo wa kusoma walio wachache. Hadhira hii haishirikishwi katika utendaji kikamilifu.
(v)	Ina historia ndefu na ndiyo maana inaitwa fasihi kongwe	(v)	Ina historia fupi, imekuja baada ya uvumbuzi wa maandishi
(vi)	Ina tanzu nyingi	(vi)	Ina tanzu chache . Hadithi fupi, tamthilia, riwaya, ushairi
(vii)	Huhifadhiwa akilini na kuwasilishwa kwake hutegemea kumbukumbu.	(vii)	Huhifadhiwa katika maandishi ambayo hubadilika
(viii)	Inabadilikabadilika kutegemea utambaji na wakati	(viii)	Haibadilikibadiliki kwani imehifadhika kwa maandishi.
(ix)	Hutegemea viziada lugha kama ngoma, ishara za uso/mwili	(ix)	Haitegemei viziada lugha.

(zozote 4 x 3= alama 12)

(c)
- Huelimisha jamii
- Hutumiwa kuburudisha jamii, kukosoa, kukejeli, nk, tabia za wanajamii ili wabadilike.
- Hutumiwa kuendeleza historia ya jamii
- Hutumiwa kuonyesha na kuendeleza thamani za jamii
- Kuimarisha ufunzaji na kipawa cha lugha
- Kuleta umoja na kujenga mahusiano bora miongoni mwa wanajamii
- Kitambulishi cha jamii

(zozote 6 x 1 = alama 6)

2. (a)
- Mzungumzaji ni Mweke
- Anazungumza na Gege nduguyeMwelusi *(alama 2)*

(b)
- Njama zimepangwa na washauri wa utemi za kumtumia Gege kumsaliti
- nduguye Mwelusi ili anyamazishwe
- Gege ameahidiwa cheo, ardhi na mali na ndoa na bintiye Mtemi
- Mipango ni kuwa harusi kubwa tayari inapangwa kumkabidhi Gege haya
- yote mradi tu amsaliti nduguye. *(alama 4)*

(c)
- Wengi ni waoga. Hata washauri wanaogopa kumweleza mtemi ipasavyo.
- Uhewala na unyenyekevu wa kupindukia. Walipenda kumpa kiongozi sifa
- za uongo
- Walipenda kutumiwa kama vile kutumbuiza

Powered By: www.manyamfranchise.com

- Walikataa kuzingatia ushauri na mawaidha km Gege
- Wengi wana ubinafsi mf. Gege, askari
- Kujipendekeza ili waonekane ni wazuri mf. Washauri wa mtemi
- Kutaka kupendelewa mf. Gege, mama Kaloo nk
- Kutii amri na kanuni za kidhalimu mf. kutotumia maji ya kisima ingawa ni
- maliasili ya umma na ni kiini cha mhai.
- Kuwasaliti wenzao mf washauri wa mtemi, Gege a
- Kusema uongo na kuwasingizia wengine mfano washauri wa mtemi

(zozote 7 x 2 = alama 14)

3. (a) **Monika**

(i) Mwenye bidii
- anafanya vizuri katika mitihani yake
- anapata udhamini kwenda ng'ambo
- anafuzu na kupata digrii

(ii) Mwenye kiburi/sodai
- anawapuuza watu wanaofika uwanjani kumlaki
- anaudharau uji wa Bi Keti
- anatumia lugha ya kifedhuli kumjibu Bi Keti
- Hana heshima kwa wazazi wake
- Anadharau Rashid anapoishi naye
- Anadharau watu wasiosoma

(iii) Amekengeuka
- Ameathiriwaina tabia za kigeni
- Anadharau utamaduni wake kw mfano ndoa za kupangiwa
- Anajiona kama mzungu ""Sisi huko ulaya hatufanyi hivi ....."

(iv) Anaupuuza wajibu wake
- Hataki kuwakimu ndugu zake na wazazi.
- Anawaacha ndugu zake wakiwa na njaa na kwenda densini.
- Mamake analazimika kwenda kikopo fedha kwa Salama/Monika
- anapokea mshahara mkubwa kumzidi.

Ana ubinafsi

(v) Mpenda starehe
- Fedha zake aziharibia kwenye mavazi na starehe
- Anapenda kwenda densi
- Anaandamana dereva wa Selemani kwa sababu hii
- Urafiki wake ni Rashid unaanzia kwenye starehe
- Amefurahi anapoalikwa kwenye hotel kubwa na Selemani/Karim
- Mfujaji

(vi) Mkaidi
- Anaonyesha ujeuri na ukaidi kwa bi keti
- Yuko tayari kupambana naye
- Hachelei kuonyesha ujeuri wake kwa wazazi wake
- Rashid anapojaribu kumdadisi anachukia.

Umuhimu wake

- Kuonyesha athari za ukengeushi katika jamii.
- Kielelezo cha yanayoweza kuwapata wato wanaopuuliza maelezi bora.
- Kuonyesha kinaya kilichopo katika maisha - Monika anapinga ndoa ya kuozwa (ya Muna na Hasani) lakini anaishia kuozwa na wazazi wake.
- Kuakisi ukweli wa methali (majuto ni mjukuu .....".
- Kielelezo cha jinsi utamaduni unavyo mdunilisha mwana mke - Anaoziwa kama adhahebu ya kuasi.

(Sifa zozote 5 x 2 = 10)

B **Muna**

(a) Mwenye heshima/mnyenyekevu

Powered By: www.manyamfranchise.com

- anafurahi na kuwachangamkia watu wanaomkaribisha
- anashauri babake/wazai wake kuhusu kazi
- Anakubali kuozwa na wazee

(b) Mwenye bidii
- anasoma kwa bidii sana
- anafuzu mitihani kwenda ng'ambo kuyaendeleza masomo yake.

(c) Msiri
- Anaficha hisia zake za kweli kuhusu kuozwa
- Anapokumbana na matatizo ya ndoa anajinyamazia

(d) Mvumilivu
- Anavumilia shida nyingi katika ndoa yake na Hasani.

(e) Mpenda haki
- Anapolazimika anatetea haki yake ya kuwatembelea wazai wake
- Yuko tayari kuonyesha jinsi mumewe anavyomnyima uhuru wake.

(f) Ana uthamini utamaduni wao ⇒ kukubali kuozwa

Umuhumi - kielelezo cha namna malezi/utiifu kwa wazai yanaoyoweza kuwa na athmani mbaya katika maisha ya mtoto.

(a) Kuonyesha jinsi wanawake wanavyo dhalilishwa..... katika asai ya ndoa/kuozwa /kuishi katika ndoa yenye mateso.

(b) Kuonyesha kiunyume cha Monika/yaani anatumiwa kama ulinganuzi (contrast) wa Monika ⇒ si mkaidi/hana kiburi/hajakengeuka/ana heshima. ***(Sifa zozote 5 x 2 = 10)***

4. Siku ya mganga

1. (a) Mganga Mwaibale anawaza haya anapotembelewa na mgonjwa mwenye dalili za ugonjwa uliomwua mke wake licha ya matibabu ya mganga. Dalili za ugonjwa huu ni pamoja na kuharisha, kukonda na kunyonyoka nywele. Ingawa mganga haujui ugonjwa huu anajitia kuutibu. Mgonjwa naye hajui udhaifu wa mganga. ***(alama 2)***

(b)
- Hajui magonjwa wanayougua wateja lakini hataki kuwambia
- Nia yake ilikuwa kunufaika kwa malipo
- Uaguzi wake wa madoido tu bali haukugundua ugonjwa halisi
- Alitoa aina ile ile ya dawa kwa magonjwa na matatizo ya kila namna mfano: kupata cheo, kurudisha mume na kumnasa mume wa wenyewe alikisia tu ugonjwa wa mgonjwa mahututi bila kupata maelezo yoyote
- Mganga mwenyewe anakiri kuwa hakuwaambia wagonjwa ukweli. Mfano,: kuhusu wembe na shida ya Asteria na rafiki yake
- Ni vigumu kuamini jinsi gani chango ingeimarisha mapenzi kuzuia uadui au kumfanya mtu apate cheo.
- Amerithi tu uganga haonyeshi dalili ya utaalamu.
- Kujidai kuwazindika wateja kwa hatari yoyote. ***(alama 10)***

(c)
- Kueneza maaambukizi ya Ukimwi kwa kuwachanja wagonjwa kwa wembe mmoja.
- Uharibifu wa mazingira kwa kutumia mimea kwa fujo
- Kuwapotosha watu kuwa angeweza kuwasaidia kupata madaraka au Mapenzi kwa dawa.
- Uongo uliwapofusha watu wasitafute tiba hospitali
- Kupata pesa na mali kutoka kwa watu kwa kutumia hila
- Aliwapotezea wateja wakati kwenda huko mbali mbugani alikokuwa.

Powered By: www.manyamfranchise.com

- Kinga aliyowapa watu dhidi ya maadui ingeweza kusababisha uhasama baina ya watu. *(alama 8)*

5. (a)
   - Mavitu alichukua hatua nyingine
   - Kumshawishi mkewe Sakina kuacha kazi ya ualimu-mwenyewe kuacha kazi ya kuajiriwa mjini.
   - Kufanya kazi za kibarua sokoni na hatimaye kwa majirani kufanya kazi ya kulipwa kwa mwezi - aliajiriwa na jirani kule kijijini
   - Kukopa pesa mara kwa mara kwa mwajiri wake
   - Kurudi kushiriki kazi za vibarua na mkewe
   - Kuwaachisha watoto wa kwanza wawili shule. Wa kiume akaandamana naye kazini na msichana akawa mlezi kwa jirani.
   - Kujinyonga *(alama10)*

   (b) Athari
   - Walihamia kijijini na mkewe hakuendelea kitaaaluma
   - Kukosa pato la kutegemea - huu ulikuwa mwanzo wa shida za kinyumbani
   - Shida zinazidi kuongeseka
   - Inakuwa vigumu kusubisi hadi mwisho wa mwezi
   - Mwajiri anambambikizia madeni na mwishowe anammegea mwajiri shamba.
   - Kuathirika kwa afya yake na shida kuwa sugu
   - Kuwaharibia watoto maisha ya baadaye, mfano, yule wa kike anatungwa mimba.
   - Mkewe Sakina anazinduka na kuanza kutafuta namna ya kuendelea na taaluma yake.
   - Kujinyonga na kumwacha mkewe mjane na watoto wake bila baba.

   (Zozote 10 x 1 = 10)

6. (a)
   - Ni silaha/kinga
   - Ni ngome ya hishima/taadhima
   - Ukweli huridhisha
   - Ukweli hupatanisha *(4 x 1· = alama 4)*

   (b) Stiari : Haki kuziangusha
   - Tashhisi - Lakinga mbele na nyuma
   - Tabdila - hifadha *(2 x 2 = alama 4)*

   (c) Ilo - inkisari
   Muongosha, kuhadaisha - tabdila
   hishima - lahja *(alama 4)*

   (d) Ni haki kudanganya kwanza unapopatanisha, pili unapotaka kuhifadhi ndoa au vitani. Katina miktadha mingine dumu katika ukweli. *(alama 4)*

   (e) (i) Kabisa *(alama 1)*
   (ii) Ukiwa katika kesi tubu ama useme ukweli: Mola atakusaidia. *(alama 2)*
   (iii)
   - Wamewafanya wasadiki
   - Wamewafanya waunge mkono *(alama 1)*

Powered By: www.manyamfranchise.com

7. (a)

- Mkulima ambaye ni nguzo ya Afrika ni kama mtumwa.
- Anateseka, ana huzuni na hana matumaini
- Baadaye matumaini yanaweza kwisha
- Kuna siku ambapo atafahamu haki yake na aidai
- Wanaomtesa wataadhibiwa. *(yoyote 4 x 1 = alama 4)*

(b) (i) Tashbihi

- Kama kuni
- Kama bahari

(ii) Kweli kinzani: Mtumwa wa watumwa waliyoridhiya

(iii) Tashhisi:

- Pumzi zilizozima taa za Afrika
- Amekita jembe lake akilisujudia *(alama 4)*

(c)

- Beti tano
- Mishororo haitoshani
- Shairi huru
- Vina vya nje vipo *(3 x 1 = alama 3)*

(d) Mshangao, masikitiko kuwa aliye nguzo ya Afrika ni mtumwa wa watumwa *(alama 2)*

(e) (i) Wakati atakapozinduka na kuidai haki yake

(ii) Kutuliza hasira za matakwa/matatizo yake hata kama ni kidogo *(2 x 2 = alama 4)*

(f) (i) Umbo

(ii) Uliokauka

(iii) kumwingisha/kumtopesha *(3 x 1 = alama 3)*

Powered By: www.manyamfranchise.com